

HALMASHAURI YA MJI WA KONDOA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Halmashauri ya Mji wa KondoA)

Simu: +255 712264912

Nukushi: +255 262360313

Barua pepe: td@kondoatc.go.tz

Tovuti: www.kondoatc.go.tz



Mkurugenzi wa Mji

S.L.P 711,

KONDOA.

TAARIFA YA KITENGO CHA SHERIA

1.0 UTANGULIZI

Kitengo cha sheria ni moja ya vitengo katika Halmashauri lengo kuu la kitengo hiki ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria yote ndani ya Halmashauri na kusimamia kesi zinazoihusu halmashauri.

2.0 MAWASILIANO YA WATUMISHI KITENGO CHA SHERIA

SN	JINA	CHEO	NAMBA YA SIMU
1	Adv.Edward R. Mhina	Mwanasheria	0754002708
2	Shabani N. Sued	Mwanasheria	0685342625

3.0 KAZI ZA KITENGO

Kitengo cha Sheria kinafanya kazi zifuatazo

1. Kusimamia na kutoa mafunzo katika mabaraza ya kata katika utatuzi wa migogoro ya ardhi na utoaji haki kwa mabaraza 8 hivyo kufanikisha kutolewa kwa maamuzi yenye tija.
2. Kupitia mikataba mbalimbali ya Halmashauri na kutoa ushauri wa kuiboresha inapobidi
3. Kutoa elimu juu ya kodi mbalimbali na ushuru unaotowwa na Halmashauri kwa wananchi, wenyeviti wa mitaa na vitongoji,

watendaji wa kata na Waheshimiwa Madiwani hivyo kupelekea kuongeza mapato ya Hamashauri.

4. Kusimamia sharia ndogo za Halmashauri kwa kushirikiana na Idara nyingine na hivyo kuleta tija na kuongeza mapato ya Halmashauri.
5. Kuiwakilisha Halmashauri katika mashauri mbalimbali mahakamani. Halmashauri inapokea mashauri mbalimbali ambayo baadhi bado yanaendelea mahakamani na mengine yameshatolewa maamuzi.

4.0 HUDUMA ZINAZOTOLEWA KATIKA KITENGO CHA SHERIA

Kitengo hiki endapo mwananchi atakitembelea atapata huduma mbalimbali ikiwemo.

1. Kutoa ushauri wa kisheria kwa jamii pale panapokuwa na uhitaji ili kupunguza migogoro miongoni mwa jamii
2. Kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kufuata na kuzingatia sharia ndogo zilizotungwa na halmashauri kwa ushirikiano wa wananchi wenyewe.

5.0 MATARAJIO YA IDARA

Kitengo kinatarajia kufanya yafuatayo kwa mwaka wa fedha 2017/18 na 2018/19

1. Kuongezaufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria kwa Halmashauri na jamii nzima kwa ujumla ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima.
2. Kutoa miongozo ya kisheria kwa mabaraza ya kata ili kupunguza changamoto za kisheria katika mabaraza.

KARIBUNI WANANCHI KATIKA KITENGO CHA SHERIA